USAFIRISHAJI



Karani wa kampuni ya mabasi ya Chaula, Said Jumanne (kulia) akimkatia tiketi kwa njia ya elektroniki abiria aliyefika katika ofisi za kampuni hiyo zilizopo katika kituo cha mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani cha Ubungo jijini Dar es Salaam jana. Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (Latra), waliagiza wamiliki wa vyombo vya usafiri kuanza kutoa tiketi kwa njia ya elektroniki kuanzia Januari 06, 2021, hata hivyo kumekuwa na changamoto ya mfumo huo kutofanya kazi kwa ufanisi, pamoja na wamiliki wa vyombo hivyo vya usafiri kutokuwa na elimu ya utumiaji wa mashine hizo. **Picha Maktaba**

# Tiketi za kielektroniki bado mfupa mgumu

Devotha Kihwelo, Mwananchi
dkihwelo@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Licha ya uwepo wa mifumo ya kisasa ya tiketi za kielektroniki na masharti ya kisheria yanayosimamia usafiri wa mabasi ya masafa marefu, changamoto katika utekelezaji wa sheria hizo imeendelea kuchochea ulanguzi wa tiketi, hususan katika vipindi vya mahitaji makubwa ya usafiri kama msimu wa sikukuu.

Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (Latra) imebaini ukiukwaji wa taratibu za usajili wa abiria katika baadhi ya mabasi, hali inayosababisha kutokuwapo kwa takwimu sahihi za wasafiri, kuhatarisha usalama wao na kuacha mianya ya upotevu wa mapato kwa wamiliki wa mabasi na Serikali.

Akizungumza Desemba 24, 2025 wakati wa ukaguzi eneo la Msata, mkoani Pwani, Mkurugenzi Mkuu wa Latra, Habibu Suluo, alisema mamlaka hiyo imekuta tiketi zenye taarifa zinazokinzana kati ya maandishi ya mkono na yale yaliyosajiliwa kwenye mfumo wa kielektroniki.

"Unakuta tiketi moja ina majina matatu tofauti. Jina lililoandikwa kwa mkono ndilo abiria analoonekana nalo, lakini jina la aliyekata tiketi halipo kabisa kwenye mfumo," alisema.

Alisema hali hiyo ni hatari endapo ajali au dharura itatokea, kwa kuwa inakuwa vigumu kubaini idadi halisi ya abiria waliokuwapo ndani ya basi pamoja na utambulisho wao.

Kwa mujibu wa sheria, kila basi linapaswa kuwa na nakala tatu za manifesto ya abiria, moja hubaki kituo cha kuanzia safari, nyingine hupelekwa polisi na ya tatu hubaki ndani ya basi.

Hata hivyo, Latra inakiri kuwa utekelezaji wa matakwa hayo bado ni dhaifu katika baadhi ya maeneo.

Katika juhudi za kudhibiti changamoto hiyo, Latra imewataka abiria kutumia majina yao kamili yanayolingana na vitambulisho rasmi kama Nida, kitambulisho cha kura au cha kazi ili kuimarisha usalama na ufuatiliaji wa wasafiri.

"Tunasema wazi, matumizi ya majina yasiyo sahihi yanachochea ulanguzi wa tiketi. Hii inawapa mwanya makondakta au wahusika wengine kukata tiketi kwa bei ya chini au kwa makaratasi bila mmiliki wa basi kujua mapato halisi," alisema Suluo.

Takwimu za Latra zinaonyesha ukubwa wa changamoto hiyo. Katika kipindi cha Desemba mosi hadi Desemba 22, 2025, jumla ya abiria milioni 2.198 walisafiri nchini, huku miamala ya tiketi ikifikia Sh79 bilioni. Hata hivyo, ni Sh4 bilioni pekee zilizofanyika kwa njia ya mtandao.

Kwa wastani, malipo ya mtandao yalikuwa Sh449 milioni kwa siku, sawa na asilimia 11 tu ya miamala yote, hali inayoonyesha kuwa malipo taslimu bado yanatawala, hivyo kuongeza ugumu wa kudhibiti ulanguzi wa tiketi.

Kwa upande wa wamiliki wa mabasi, changamoto hiyo inaelezwa kuchochewa zaidi na uwepo wa watu wasiokuwa rasmi katika stendi.

Mmiliki wa mabasi ya Happy Nation, Issa Nkya, alisema ulanguzi wa tiketi hauchochewi na wamiliki wa mabasi, bali na wapigadebe na watu wanaoingilia mchakato wa uuzaji wa tiketi.

Alisema wamiliki wamekubali mabadiliko ya mfumo, wameingia kikamilifu kwenye tiketi za mtandao na wanafuata sheria, lakini bado wanapata hasara kutokana na vitendo vya ulanguzi vinavyofanywa na watu wanaojifanya mawakala.

"Latrailitwambiatukishaingia kwenye tiketi za mtandao, ulanguzi utaisha. Sisi tumeingia, lakini wapiga debe bado wapo palepale stendi," alisema.

Katibu Mkuu wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (Taboa), Priscus Joseph, alisema kutokutumiwa kwa kitambulisho cha Taifa (Nida) katika ukataji wa tiketi za kielektroniki umeacha mwanya wa walanguzi na wasafiri hewa.

"Bila uthibitisho wa Nida, mtu anaweza kukata tiketi nyingi mtandaoni, asisafiri, halafu tiketi hizo zikarudi kuuzwa stendi kwa pesa taslimu," alisema.

Alisema suala hilo liliwasilishwa mara kadhaa kwa Latra na pendekezo la msingi likiwa ni kuunganisha mfumo wa tiketi za kielektroniki na Nida ili taarifa za abiria ziwe sahihi na zisizoweza kubadilishwa.

Kwa mujibu wa Taboa, changamoto huongezeka zaidi wakati mtandao unapokuwa haufanyi kazi vizuri, hasa kwa wasafiri wa maeneo ya vijijini, hali inayoonyesha pengo kati ya maendeleo ya teknolojia na mazingira halisi ya wananchi.

"Teknolojia imeenda mbele kuliko mazingira ya wananchi wengi. Ndiyo maana utekelezaji wa sheria na upatikanaji wa Nida kwa kila Mtanzania ni suluhisho la msingi," alisema.

**"Tunasema wazi, matumizi ya majina yasiyo sahihi yanachochea ulanguzi wa tiketi. Hii inawapa mwanya makondakta au wahusika wengine kukata tiketi kwa bei ya chini au kwa makaratasi bila mmiliki wa basi kujua mapato halisi."**

Habibu Saluo

# Madereva wanne wanaswa kwa ulevi Krismasi

Juma Mtanda, Mwananchi
jmtanda@mwananchi.co.tz

**Morogoro.** Jeshi la Polisi Mkoa wa Morogoro linawashikilia madereva wanne waliokutwa wakiendesha vyombo vya moto wakiwa wamelewa wakati wa sikukuu ya Krismasi.

Pamoja na madereva hao, polisi pia wamewakamata watuhumiwa wengine wa makosa tofauti, ikiwamo umiliki wa silaha za kienyeji na kujihusisha na biashara haramu ya wanyamapori.

**20**

**Idadi ya vipande vya nyama ya tohe anavyodaiwa kukamatwa navyo mkazi wa Ifakara.**

Hayo yameelezwa leo Ijumaa, Desemba 26, 2025, na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Alex Mkama, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Kamanda Mkama amesema madereva hao walikamatwa baada ya kubainika wakiendesha vyombo vya moto wakiwa na viwango vya juu vya ulevi, hali inayohatarisha usalama wao pamoja na watumiaji wengine wa barabara.

Amewataja waliokamatwa kwa ulevi ni Alexander Mapunda (45) aliyedaiwa kulewa kwa kiwango cha 667.4 mg/100ml, Theodory John (33) aliyedaiwa kulewa kwa 171.4 mg/100ml, Kibaya Simon (31) aliyedaiwa kulewa kwa 408.9 mg/100ml na Yona Agustino (28) aliyedaiwa kulewa kwa 776.8 mg/100ml.

"Operesheni ilifanyika jana Desemba 25, 2025 Manispaa ya Morogoro na maeneo mengine ikiwa ni sehemu ya juhudi za Polisi kuhakikisha usalama wa raia na mali zao katika kipindi cha sikukuu unaimarishwa," alisema Mkama.

Katika matukio mengine, alisema katika Kata ya Katindiuka Wilaya ya Kilombero, mkazi wa Ifakara, Hussein Rashid (40), alikamatwa akiwa na silaha ya kienyeji aina ya gobole, risasi saba kinyume cha sheria na vipande 20 vya nyama ya tohe.

"Silaha nyingine aina ya gobole ilitelekezwa na wahalifu waliokuwa wakifuatiliwa na askari katika eneo la Chamwino Manispaa ya Morogoro na Jeshi la Polisi linatoa wito kwa wananchi kuendelea kushirikiana na vyombo vya dola kwa kutoa taarifa za uhalifu bila ya kuwa na ushirikiano polisi haiwezi kutekeleza majukumu ya kuzuia na kudhibiti wahalifu ili kudumisha amani na usalama wa nchi yetu," alisema.

